TANGAZO LA SERIKALI Na……la Tarehe……

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ZA MWAKA 2017

YALIYOMO

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Eneo la matumizi
3. Tafsiri.
4. Utozaji wa Ada na Ushuru
5. Muda wa kulipa Ada na Ushuru
6. Wajibu wa Mfanyabiashara
7. Ukusanyaji wa madeni ya Ada na Ushuru
8. Kukamata na kuuza mali
9. Mamlaka ya kuingia
10. Uteuzi wa Wakala
11. Wajibu wa Wakala
12. Makosa ya Wakala
13. Kibali cha ujenzi
14. Masharti kuhusu Mabango ya biashara
15. Kibali cha kununua mazao mchanganyiko
16. Uwezo wa Mkurugenzi kufifilisha kosa
17. Makosa na Adhabu
18. Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na…….

MAJEDWALI.

JEDWALI LA KWANZA:

A. Ushuru wa mazao
B. Ushuru wa Machinjio
C. Ada ya ukaguzi wa Nyama
D. Ushuru wa kushusha mizigo katika eneo au sokololote lililotengwa na Halmashauri

E. Ushuru wa tandiko/meza au kizimba kwa bidhaa mbalimbali katika soko, Minada, Magulio na maeneo mengine yaliyotengwa na Halmashauri.
F. Ada ya kibali.
G. Ada ya zabuni.
H. Ada za kukodi mali za Halmashauri
I. Ushuru wa standi na maegesho katika maeneo mengine ya umma
J. Ushuru wa Mabango
K. Ushuru wa madini y aujenzi.
L. Kodi ya pango na majengo mengine ya Halmashauri.
M. Ada ya usajili wa magari ya biashara au mizigo.
N. Ada za huduma za ardhi.

JEDWALI LA PILI
Rejista ya wafanyabiashara
JEDWALI LA TATU
Fomu ya kukamata mali
JEDWALI LA NNE
Kibali cha ujenzi
JEDWALI LA TANO
Fomu ya maombi ya kibali cha kubandika mabango ya biashara.
JEDWALI LA SITA
Fomu ya maombi ya kibali cha kununua mazao mchanganyiko
JEDWALI LA SABA
Fomu ya kukiri na kufifilisha kosa

SEHEMU YA I

UTANGULIZI

Jina	1.	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Matumizi	2.	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.
Tafsiri	3.	Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo;-
		"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni

mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

"Kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

"Kituo cha Mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

"Madini ya ujenzi" maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"Maegesho'' Sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda.

"Masoko" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa.

"Mnada" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

"Ushuru wa Madini ya Ujenzi" maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa Kokoto, Mawe, Changarawe,

Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

SEHEMU YA II

NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni:-

i. Ada ya kukodisha mali za Halmashauri,
ii. Ada ya machinjio, ukaguzi wa nyama na ushuru wa Bucha,
iii. Ushuru wa Mazao mchanganyiko,
iv. Ada na Ushuru wa Mazao ya Biashara
v. Ushuru wa stendi na maegesho,
vi. Ushuru wa Samaki,
vii. Ushuru wa madini ya ujenzi,
viii. Ada ya kuendesha shughuli za utamaduni, burudani na michezo,
ix. Ada ya matangazo ya biashara,
x. Ada ya upimaji wa ardhi na vibali vya ujenzi.
xi. Ada na Ushuru kwa huduma nyingine
xii. Ada ya maombi ya zabuni.
xiii. Ada ya mkataba

(4) Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru kutokana na chanzo husika.

(5) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

(3) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri/ Wakala na mlipa Ada na ushuru.

Uteuzi wa Wakala

6. (1) Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa Wakala

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya sheria ndogo hizi atakuwa na wajibu wa;

(a) kukusanya na kupokea Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) Wakala aliyeteuliwa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kusaini Mkataba.

(d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unahusika na Mkataba.

(e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano (5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala kwa kila mwezi;

(f) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

SEHEMU YA III

MAKOSA NA ADHABU

Makosa na Adhabu

7. Itakuwa ni kosa :-

(1) Kwa Wakala;

(a) kukusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b) kujaribu au kukusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;

(c) kushindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

Wakala atakayetenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi Hamsini elfu (50,000/=) na isiyozidi shilingi Laki Tatu (300,000/=) au Kifungo cha miezi kumi na miwili jela au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Kwa yeyote;

(a) Atakayeshindwa, atakayedharau, au atakayekaidi/ Atakayekataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Atakayeshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) Atakayetengeneza, atakayetayarisha, atakayeidhinisha utengenezaji, au atakayetunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) atakayeshindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; Na

(f) Atakayemzuia Afisa Muidhiwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Mtu atakayetenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungu shilingi hamsini elfu (50,000/=) na isiyozidi shilingi Laki Tatu (300,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi Miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

8. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi Laki moja (100,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hizi.

Sheria zilizofutwa

9. Sheria ndogo hizi zinafuta:-

(a) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Ushuru wa Shughuli za Utamaduni) za Mwaka 2001, GN. No. 09/2001

(b) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Ushuru wa Magulio ya mazao mchanganyiko ya kilimo) za Mwaka 2006, GN. No.248/2006.

(c) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Ada za Vibali vya Ujenzi) za Mwaka 2001, GN. No. 09/2001

(d) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya (Ushuru wa Mazao) Mwaka 2004 GN. Na. 68/2004

(e) Sheria Ndogo Halmashauri ya Wilaya Shinyanga (Ada za Vibao vya matangazo ya biashara) za mwaka G.N. Na.336 A 2005

(f)

(g) Sheria Ndogo Halmashauri za Wilaya Shinyanga (Magulio)

YAMEUNDWA CHINI YA KIFUNGU CHA 4 (1)

JEDWALI LA KWANZA

I. ADA YA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

Na.	Huduma	Kiwango
1	Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya mikutano/ vikao na sherehe	Kwa mujibu wa Mkataba
2	Kukodi viti	Kwa mujibu wa Mkataba
3	Kukodi Gari: Magari madogo	Kwa mujibu wa Mkataba
	Magari makubwa	
4	Mitambo (Trekta, Total station, Vifaa vya GPS na kadhalika)	Kwa mujibu wa Mkataba
5	Vibanda vya biashara mzunguko wa Stendi	Kwa mujibu wa Mkataba
6	Vibanda vya biashara sokoni	Kwa mujibu wa Mkataba
7	Mali nyingine za Halmashauri	Kwa mujibu wa Mkataba

II. ADA NA USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

Na	***zao***	***Kiwango***
1	Viazi	3% ya Bei ya kununulia
2	Vitunguu maji/Matunda/Karoti/Kabichi/ Nyanya	3% ya Bei ya kununulia
3	Maharage/ Karanga / Mchele	3% ya Bei ya kununulia
4	Mazao ya Mboga	3% ya Bei ya kununulia
5	Mahindi/Alizeti/Uwele/Mtama/Mpunga/ Udaga na mazao mengine	3% ya Bei ya kununulia

III. ADA NA USHURU MAZAO YA BIASHARA

Na.	*Zao*	*Kiwango*
1	Pamba	5% ya Bei ya kununulia
2	Mkonge	3% ya Bei ya kununulia
3	Choroko	3% ya Bei ya kununulia

IV. ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA

Na	*Ada/ushuru*	*Kiwango*
1	Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe atakayechinjwa	2,500/= kila mmoja
2	Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Kondoo, Mbuzi na Nguruwe atakayechinjwa	1000/= kila mmoja
3	Kuwamba na kukausha ngozi	300/= ngozi
	(a) Ng'ombe	100/= kwa ngozi
	(b) Mbuzi, Kondoo	
4	Ushuru wa Bucha la Ng'ombe Mbuzi, Kondoo, (Mnadani).	300/= kwa mfugo
5	Ada ya kusafirisha ngozi	
	(a) Ng'ombe	300/= kwa ngozi
	(b) Mbuzi, Kondoo	100/= kwa ngozi

V. USHURU WA MAUZO YA MIFUGO MINADANI

Na	*Aina ya Mnyama*	*Kiwango*
1	Ng'ombe Mnada wa Mhunze	1000/= kwa ng'ombe
2	Ng'ombe Minada mingine isipokuwa Mhunze	5000/= kwa ng'ombe
3	Mbuzi Mnada wa Mhunze	600/= kwa mbuzi
4	Mbuzi Minada Mingine isipokuwa Mhunze	1500/= kwa mbuzi
5	Kondoo Mnada wa Mhunze	600/= kwa kondoo
6	Kondoo Minada mingine isipokuwa Mhunze	1500/= kwa kondoo
7	Ushuru wa Kuku	1000/= kwa tenga
8	Wanyama Wengine	1500/= kila mnyama

VI. ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

Na	***Ada/Ushuru***	***Kiwango***
1	Kibali cha ngoma	30,000/=kwa onesho

2	Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho (Sinema, video, maigizo, sarakasi, ngoma n.k	25,000/= Kwa onesho
3	Kibali cha kuchezesha Michezo ya Kubahatisha	30,000/= Kwa kibali
4	Kibali cha Mechi za Mipira	10% ya Mapato kwa kila mechi
5	Ada ya video au sinema	60,000/= kwa onesho
Na.	**A. Shughuli za Tiba**	
1	Waganga toka nje ya Wilaya	50,000/= kwa Mwaka
2	Waganga maarufu ndani ya Wilaya	20,000/= kwa Mwaka
3	Waganga wadogo ndani ya Wilaya	10,000/= kwa Mwaka
4	Kibali cha kuuza dawa za asili	10,000/= kwa Mwaka

VII. ADA NA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA

Na	Chombo cha usafiri	Ushuru wa Maegesho
1	Pikipiki iliyosajiliwa kwa Biashara katika maeneo yaliyotengwa	500/= kwa siku
2	Teksi	1000/= kwa siku
3	Lori chini ya tani 7/ Pick up/ Basi dogo	3,000/= kwa siku
4	Lori zaidi ya Tani 7/ Basi kubwa	4,000/= kwa siku
5	Magari mengine yasiyo ya biashara	500/= kwa siku
6	Ushuru wa kituo cha mabasi/stendi	
	(a) Mabasi makubwa zaidi ya abiria 25	3,000/= kwa siku
	(b) Mabasi yanayobeba abiria chini ya 25	1,500/= kwa siku

VIII. ADA YA MATANGAZO/MABANGO YA BIASHARA

Na	*Aina ya Tangazo*	*Kiwango cha ushuru kwa mwaka*
1	Ada ya Tangazo lenyewe	3,000/= kwa maombi
2	Matangazo yanayong'aa	8,000/= kwa kila mita moja ya mraba
3	Matangazo yasiyong'aa	6,000/= kwa kila mita moja ya mraba
4	Matangazo yanayotoa na yasiotoa Mwanga yasiyofikia mita moja kwa mraba.	4,000/= Kwa tangazo
5	Tangazo kwa kutumia kitambaa	5,000/= kwa tukio

6	Matangazo ya vipaza Sauti/ Magari na Promosheni	20,000/= kwa kibali

IX. ADA YA UPIMAJI WA ARDHI NA VIBALI VYA UJENZI

Na	*Ada ya Kibali cha Ujenzi/ Upimaji*	*Kwa kila kibali*
1	Mnara wa simu	500,000/=
2	Ghorofa moja	120,000/=
3	Nyumba za Biashara	50,000/=
4	Nyumba ya Makazi	20,000/=
5	Kituo cha mafuta	250,000/=
6	Majengo ya Taasisi Binafsi	150,000/=
7	Maghala na Bohari.	100,000/=
8	Ujenzi wa Uzio	100/= kwa "Sq meter
9	Majengo ya Ibada	100,000/=
10	Vituo vya Utalii/Mapumziko	250,000/=
11	Majengo ya Viwanja	500,000/=
12	Viwanda Vidogo Vidogo vya Huduma	250,000/=
13	Vituo vya Mafuta	250,000/=
Na	**Ada na mabadiliko (alteration) ya Jengo**	**Kwa kibali**
1	Nyumba ya kuishi na biashara	40,000/=
2	Nyumba ya Biashara	60,000/=
3	Nyumba ya kuishi	30,000/=
4	Ghorofa	150,000/=
5	Kiwanda, Bohari, Ghala	100,000/=
6	Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Makazi)	20,000/=
7	Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Biashara)	50,000/=
Na.	**Ada za Huduma ya Ardhi**	**KIWANGO**
1	Mchoro wa upimaji	10,000/= kwa kila mchoro
2	Kutambua eneo (Plot identification)	10,000/= kwa kila plot
3	Kurudishia mawe yanaonesha mipaka (Beacon replacement)	5,000/= kwa kila jiwe

X. USHURU WA HOTEL (Hotel Levy)

Na	*Aina ya Biashara*	*Kiwango*
1.	Hotel	10% ya mauzo kila chumba kwa siku

XI. ADA NA USHURU WA HUDUMA NYINGINE

Na.	*Ada*	*Kiwango*
1	Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa Baa, Hoteli na Migahawa na maeneo mengine ya kutoa huduma za vyakula au vinywaji kwa umma.	10,000/= kwa miezi mitatu
2	Ushuru wa kuhifadhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura ovyo.	3000/= kwa mnyama kwa siku
3	Faini ya kutovaa sare kwa wahudumu wa Bar/ Mgahawa/Hotel na maeneo mengine ya kutoa huduma za vyakula au vinywaji kwa Umma	20,000/= kwa siku
4	Ada ya Maombi ya kusajili vyama vya ushirika	30,000/= kwa ombi
5	Ada ya usajili vikundi vya jamii	11,000/= kwa ombi
6	Ada ya usimamizi wa asasi za Umwagiliaji	20,000/=kwa ombi
7	Ada ya maombi ya hati ya ukomo wa madeni	50,000/=kwa ombi
8	Ada ya kukagua hesabu za shule za Sekondari Binafsi	100,000/=kwa ombi
9	Ada ya pango la ardhi kwa wamiliki wa maeneo yaliyopangishwa Minara ya Simu	5% ya alicholipwa
10	Mauzo ya vitabu vya stakabadhi za fedha za shule za Serikali na Vijiji.	5000/= kwa kitabu
11	Mauzo ya Hati za Malipo vijijini.	20,000/= kwa ombi
12	Mauzo ya vitabu vya hati za malipo shule za Msingi na Sekondari	15,000/=kwa kitabu
13	Mauzo ya Vitabu vidogo vya Ushuru mbalimbali	5000/=kwa kitabu
14	Kukodisha vifaa vya muziki vya Halmashauri	250,000/= kwa siku
15	Ushuru wa kufanya biashara katika eneo la Halmashauri ngazi ya Kata	2000/= kwa siku
16	Vitabu vya ushuru wa Hotel	20,000/=

XII. MAOMBI YA ZABUNI

Na	*ombi*	*kiwango*
1	*Maombi ya ushuru wa mapato*	*50,000/= kwa kila ombi*
2	*Maombi ya kutoa huduma mbalimbali*	*50,000/= kwa kila ombi*
3	*Maombi ya kai za ujenzi*	*100,000/= kwa kila ombi*

XIII. USHURU WA MADINI YA UJENZI

Na	Aina ya Madini	Tani	Kiwango Tsh.
1	Mchanga/Kokoto /mawe kifusi	1-3½	1,500/=
2	Mchanga /Kokoto/mawe/kifuzi	3½ -7	2,000/=
3	Mchanga /kokoto/mawe/kifusi zaidi ya	7	2,500/=

XIV. ADA YA MIKATABA

Na	Thamani ya Mkataba	Kiwango
1	Mkataba wa thamani kuanzia Tshs 1 – 50,000,000/=	Tshs 50,000/= kwa kila mkataba
2	Mkataba wa thamani kuanzia Tshs 50,000,000/= hadi Tshs 250,000,000/=	Tshs 150,000/= kwa kila mkataba
3	Mkataba wa thamani kuanzia Tshs 250,000,000/= na kuendelea	Tshs 300,000/= kwa kila mkataba

XV. ADA YA KUPITISHA BOMBA LA MAJI KATIKA BARABARA ZA HALMASHAURI.

Na	**Aina barabara**	**Kiwango**
1	Barabara ya changarawe	200,000/=kwa ombi
2	Barabara ya udongo	150,000/= kwa ombi

XVI. USHURU WA KUFANYA BIASHARA KATIKA MAGULIO/MINADA

Na	**Aina Ya Bidhaa**	**Kiwango**

1	Mitumba	1,000/= kwa mfanyabiashara
2	Vyombo vya nyumbani	1,000/= kwa mfanyabiasha
3	Nguo za dukani	1,000/= kwa mfanyabiahara
4	Biashara nyinginezo ambazo hazikutajwa	1,000/= kwa mfanyabiashara

XVII. ADA YA KUKODISHA MITAMBO NA MAGARI YA HALMASHAURI BILA POSHO YA DEREVA

Na	**Aina gari/mtambo**	**Kiwango**
1	Lori tani 7	Itategemea gharama za uendeshaji wa gari kwa kipindi husika.
2	Trekta	Kwa mujibu wa Makubaliano
3	Grender	Kwa mujibu wa Makubaliano
4	Exavetor	Kwa mujibu wa Makubaliano
5	Roller	Kwa mujibu wa Makubaliano

JEDWALI LA PILI

ORODHA YA MASOKO NA MAGULIO

(Chini ya kifungu cha 4 (4))

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga umebandikwa katika Sheria ndogo hizi kufuatia azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya

ya Shinyanga ulioitishwa kihalali na kukutana tarehe 31/08/2016 na umebandikwa mbele ya:-

……

NGASSA S. MBOJE

MWENYEKITI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU

……..

Bakari K. Mohamed

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU

NATHIBITISHA,

……

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS-TAMISEMI

DODOMA

Tarehe……

HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 8)

Mimi …….. nakiri mbele ya …….....ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kishapu, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Ada na Ushuru) za Mwaka 2017.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……. ya Mwezi…… Mwaka …….20……..

Jina……..

Saini……

Mbele ya :

Jina: ……..

Cheo: ……

Saini: ……